**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI**

**01** **KISWAHILI**

**Muda: Saa 1:40** **Mwaka: 2021**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **arobaini na tano (45)**.
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.
3. Soma maelekezo yote yaliyoko katika **fomu maalum ya kujibia (OMR)**.
4. Jaza taarifa zote katika fomu ya OMR.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** kisha **weka kivuli** kwenye **tarakimu** za namba hiyo mahali panapohusika kwenye karatasi yako ya kujibia.
6. Weka **kivuli** kwenye herufi ya jibu lililo sahihi kwa swali 1 – 40. Kwa mfano, kama jibu sahihi ni A weka kivuli kama ifuatavyo:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| [A] | [B] | [C] | [D] | [E] |

7. Ukigundua kuwa herufi uliyowekea kivuli **si jibu sahihi** futa kivuli hicho kwa umakini kwa kutumia **kifutio safi** kabla ya kuweka kivuli katika herufi mpya.
8. Tumia **penseli ya HB** tu katika kujibu swali la 1 – 40; na kalamu ya wino wa **bluu** au **mweusi** kwa swali la 41 hadi 45.
9. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.



Scanned with CamScanner

## SEHEMU A (Alama 35)

Sikiliza kwa makini hadithi utakayosomewa na msimamizi, kisha jibu swali la 1 - 5, **kwa kuweka kivuli katika herufi ya jibu lililo sahihi** katika fomu yako ya kujibia.

**Maswali**

1. Malkia wa nyuki alikuwa analindwa na nani?
   A Vibaraka B Askari hodari C Wanakijiji D Nyuki Hohehahe E Wafanyakazi.

2. Ni kitu gani ambacho malkia wa nyuki hakukipenda?
   A Wanakijiji hohehahe
   B Mafundi wa masega
   C Ushirikiano wa nyuki
   D Vibaraka wa malkia
   E Kuwalipa vibarua

3. Nani alijishughulisha kutafuta nekta kwenye maua?
   A Nyuki wote
   B Vibarua
   C Wafanyakazi
   D Vibaraka
   E Wanakijiji

4. Utajiri katika kijiji cha nyuki ulitokana na nini?
   A Kuuza asali B Kuuza nta C Kuuza masega D Kuuza maua E Kuuza mizinga

5. Nani walitumika kupeleka habari mbalimbali katika vijiji vya jirani?
   A Vibarua B Wafanyakazi C Vibaraka D Wanakijiji E Nyuki

Katika swali la 6 - 35, **weka kivuli katika herufi ya jibu lililo sahihi** katika fomu yako ya kujibia.

6. Wanakijiji walifanya juu chini ili kuleta maendeleo katika kijiji chao. Nahau "fanya juu chini" inafafanuliwa na kifungu kipi cha maneno kati ya vifuatavyo?
   A Walijitahidi kwa kila njia.
   B Walishirikiana kwa pamoja.
   C Walijituma kwa ujasiri.
   D Walijituma kwa uzalendo.
   E Walitumia nguvu.

7. Nahau ipi yenye maana ya "kunywa pombe?"
   A Piga mbizi B Piga chenga C Piga yowe D Piga soga E Piga maji

8. Katika sentensi "Dada alimwambia kuwa atakapopata muda atakuja nyumbani," mzungumzaji ametumia nafsi gani kati ya hizi?
   A Nafsi ya pili wingi
   B Nafsi ya tatu wingi
   C Nafsi ya tatu umoja
   D Nafsi ya pili umoja
   E Nafsi ya kwanza wingi



Scanned with CamScanner

9. "Sisi ni wanafunzi hodari wa somo la Kiswahili." Kauli hiyo inawakilisha nafsi ipi kati ya hizi zifuatazo?

A Nafsi ya kwanza umoja
B Nafsi ya tatu wingi
C Nafsi ya tatu umoja
D Nafsi ya kwanza wingi
E Nafsi ya pili wingi

10. "Daktari alisema kwamba mgonjwa wetu amepata ahueni.'' Hiyo ni aina gani ya kauli kati ya zifuatazo?

A Tata
B Mazoea
C Halisi
D Taarifa
E Kutenda

11. Masumbuko aliwaambia kuwa, hataingia darasani tena. Kauli halisi ya sentensi hii ni ipi kati ya zifuatazo?

A Masumbuko aliwaambia kuwa, "haingii darasani tena."
B Masumbuko aliwaambia, "hataingia darasani tena."
C Masumbuko aliwaambia, "sitaingia darasani tena."
D Masumbuko aliwaambia, "hakuingia darasani tena."
E Masumbuko aliwaambia "kamwe haingii darasani."

12. "Nyamante alikata shauri na kuwaambia wenzake, kweli elimu ndiyo mkombozi wa mtoto wa kike." Nahau "kata shauri" katika sentensi hii ina maana ipi kati ya zifuatazo?

A Kuamua
B Kuwatahadharisha
C Kuwaasa
D Kuonya
E Kufundisha

13. Chekacheka anapenda watoto wake wawe na tabia njema hadi ukubwani. Methali ipi kati ya zifuatazo inahimiza tabia ya aina hiyo?

A Zimwi likujualo halikuli likakwisha.
B Asiyesikia la mkuu huvujika guu.
C Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.
D Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.
E Tabia hupamba kuliko libasi.

14. "Nikitembea walio wafu huamka na walio hai hukaa kimya." Jibu la kitendawili hiki ni lipi kati ya yafuatayo?

A Nyuki ndani na nje ya mzinga
B Yai na kifaranga chake
C Majani makavu na mabichi
D Kulala usingizi na kuamka
E Tumbo na chakula

15. Ni methali ipi kati ya zifuatazo ina maana sawa na methali "akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki?
   A Baniani mbaya kiatu chake dawa.
   B Damu nzito kuliko maji.
   C Undugu kufaana si kufanana.
   D Shukrani ya punda mateke.
   E Sikio la kufa halisikii dawa.

16. Neno lipi kati ya yafuatayo ni jumuishi kwa maneno haya "nyanya, vitunguu, pilipili na tangawizi?"
   A Nafaka B Matunda C Vinywaji D Vitoweo E Viungo

17. Mwaka 1985 Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliamua kung'atuka madarakani na kumwachia Mheshimiwa, Ali Hassan Mwinyi. Kitendo cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kung'atuka kinamaanisha nini?
   A Kuaga wafanyakazi
   B Kuwaachia wafanyakazi
   C Kustaafu kazi
   D Kujiuzulu madaraka
   E Kupumzika kazi kidogo

18. Neno lipi kati ya yafuatayo ni jumuishi kwa maneno haya "almasi, dhahabu, Tanzanaiti na lulu?"
   A Shaba B Vyuma C Marumaru D Mgodi E Madini

19. Katika neno "ninakula" kiambishi cha wakati uliopo ni kipi kati ya vifuatavyo?
   A -ni- B -ku- C -na- D -la- E -kul-

20. "Muda ulipowadia wanafunzi wote tulisimama foleni.' Neno "wadia" linashabihiana na neno lipi kati ya yafuatayo?
   A fika B kwisha C patikana D pungua E ongezeka

21. Katika sentensi "Wimbo wa Taifa umeimbwa kwa ustadi." Neno lipi kati ya yafuatayo limesimama kama kitenzi?
   A wimbo B ustadi C taifa D kwa E umeimbwa

22. Neno lipi **halilandani** na mengine kati ya maneno yafuatayo?
   A Kuku B Bata C Kaa D Mwewe E Kunguru

23. "Mtoto mzuri anajua kupangilia ratiba." Katika sentensi hii, neno lipi kati ya yafuatayo limetumika kama kivumishi?
   A mzuri B mtoto C kupangilia D ratiba E anajua



Scanned with CamScanner

24. "Hawa ndio wapole darasani mwetu." Katika sentensi hii, neno lipi kati ya yafuatayo limetumika kama kiwakilishi?

A ndio B hawa C wapole D darasani E mwetu

25. Ni neno lipi kati ya yafuatayo linakamilisha sentensi hii kwa usahihi? "Nikisoma kwa bidii _____ mtihani wangu."

A ningefaulu B nitafaulu C ningalifaulu D ningelifaulu E ninafaulu

26. "Nitakula uji wangu kesho asubuhi." Sentensi hii imekosewa. Sentensi sahihi ni ipi kati ya zifuatazo?

A Nitamung'unya uji wangu kesho asubuhi.
B Nitatafuna uji wangu kesho asubuhi.
C Nitakunywa uji wangu kesho asubuhi.
D Nitameza uji wangu kesho asubuhi.
E Nitabugia uji wangu kesho asubuhi.

27. "Kijiji chetu kina maendeleo duni lakini mwaka ujao itakua kinyume chake." Je, mwaka ujao kijiji chetu kitakuwa na maendeleo gani?

A Imara B Dhaifu C Mabaya D Hafifu E Dhahili

28. Maneno yapi kati ya yafuatayo yapo katika mpangilio sahihi kwa kuzingatia matumizi ya kamusi?

A fana, fani, faraja, farasi
B fana, faraja, farasi, fani
C fana, farasi, faraja, fani
D fani, fana, faraja, farasi
E fana, farasi, fani, faraja

29. Kitenzi kipi kati ya vifuatavyo kinatokana na nomino "mchemsho?"

A Mchemshaji B Chemsha C Chemshika D Chemshana E Chemshiana

30. Ni nomino ipi inaundwa kutokana na neno "chunga?"

A Chungana B Chungiana C Mchungaji D Chungika E Chungisha

31. "Polepole ndio mwendo." Methali hii inahusiana na methali ipi kati ya hizi zifuatazo?

A Maneno mengi hula matendo.
B Chembe na chembe mkate huwa.
C Chanda chema huvikwa pete.
D Shukrani ya punda ni mateke.
E Dua la kuku halimpati mwewe.



Scanned with CamScanner

32. Charubuma alionywa na wazazi wake kuacha tabia ya wizi, lakini hakuwasikiliza hatimaye alifungwa jela. Methali gani kati ya zifuatazo inakemea tabia hiyo isiyofaa katika jamii?

A Asiye na mwana aeleke jiwe.

B Asiye na lake hafungi safari mapema.

C Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

D Asiye na bahati habahatishi.

E Asiye na mengi ana machache.

33. "Hakuna msiba ____________". Kifungu kipi cha maneno kati ya vifuatavyo kinakamilisha methali hii?

A usiokuwa na vilio

B usiokuwa na mwenziwe

C usiokuwa na chakula

D usiokuwa na matanga

E usiokuwa na watu

34. Kirefu cha neno BAKITA ni kipi kati ya maneno yafuatayo?

A Baraza la Sanaa la Taifa

B Baraza la Mitihani la Tanzania

C Baraza la Michezo Tanzania

D Baraza la Kiswahili Tanzania

E Baraza la Kiswahili la Zanzibar

35. Katika uandishi wa kumbukumbu za mkutano saini ya mwenyekiti hukaa sehemu gani?

A Mwanzoni mwa kichwa cha kumbukumbu

B Katikati ya kumbukumbu kwenye ajenda za mkutano

C Mwishoni mwa kumbukumbu upande wa kulia

D Mwishoni mwa kumbukumbu upande wa kushoto

E Baada ya majina ya waliohudhuria na wasiohudhuria





Scanned with CamScanner

## SEHEMU B (Alama 5)

Kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku, jibu swali la 36- 40 kwa **kuweka kivuli katika herufi ya jibu lililo sahihi** katika fomu yako ya kujibia ili kukamilisha tangazo lifuatalo.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| A | saa 5:00 asubuhi | B | +255 222333767 | C | KUKATIKA KWA UMEME |
| D | Limetolewa na meneja wa TANESCO | | | E | Shirika la Umeme Tanzania |

36.________________________

37.__________________ wilaya ya Bagamoyo linapenda kuwatangazia wateja wake wote kuwa kutakuwa na tatizo la kukatika kwa umeme tarehe 13/8/2021 siku ya Jumapili, kuanzia 38. ________________ hadi saa 9:00 mchana. Sababu ya kukatika kwa umeme ni matengenezo makubwa ya kubadili nyaya katika njia kuu ya umeme. Maeneo yote ya Wilaya ya Bagamoyo yatakosa huduma ya umeme. Shirika linaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

39.____________________

Wasiliana nasi kupitia,
40. ____________________

## SEHEMU C (Alama 10)
## UFAHAMU

Soma kwa makini hadithi ifuatayo kisha jibu swali la 41 - 45 kwa **kuandika jibu sahihi** katika fomu yako ya kujibia. Tumia kalamu ya wino wa **bluu** au **mweusi**.

Hapo zamani za kale kulikuwa na Mzee Beberu na familia yake. Mzee huyo alikuwa na mke na watoto watatu ambao ni Chandachema, Mahangaiko na Shida. Mama yao alikuwa anaitwa Chakupewa. Familia yao ilikuwa tajiri. Walikuwa na mashamba lukuki, nyumba tatu, magari matatu pamoja na miradi mbalimbali. Baada ya miaka mitano kupita afya ya Mzee Beberu ilianza kutetereka. Mzee huyo alianza kuugua maradhi kadha wa kadha baada ya kupata ajali ya gari wakati akitoka kukagua miradi yake.

Mzee Beberu alikaa kitandani kwa miaka takribani mitatu baada ya kugundulika kuwa alikuwa amevunjika uti wa mgongo. Hakuwa na uwezo wa kunyanyuka mwenyewe bila msaada wa mtu mwingine. Hatimaye, Mzee Beberu **alikata kamba**. Baada ya kifo cha mzee huyo, maisha yalianza kubadilika katika familia kwa kuwa na migogoro mingi. Mahangaiko na Shida wakaanza kuwa na tabia mbaya ya ulevi na waliuza mali za familia. Miezi sita baadaye, hali ya maisha ilizidi kuwa mbaya hususan pale mali zote zilipouzwa hadi nyumba



Scanned with CamScanner

waliyokuwa wakiishi na mama yao. Mahangaiko na Shida waliondoka na kwenda kusikojulikana.

Chakupewa na Chandachema walibaki wakiishi kwa shida. Siku moja Chandachema aliongozana na mama yake msituni kutafuta kuni. Wakati wakiwa njiani mvua kubwa ilinyesha. Chakupewa alikuwa haijui vyema njia iendayo msituni hivyo, ilimlazimu kuweka alama kwa kuchuma majani na kudondosha njiani huku mwanaye akiwa anamwangalia. Kabla ya kufika msituni, Chakupewa aligongwa na nyoka. Hivyo, Chandachema alilazimika kumbeba mama yake na kurudi naye nyumbani ili kumpeleka hospitali. Chakupewa alipelekwa hospitali na kupata matibabu, akapona. Hatimaye alirudi nyumbani na kuendeleza maisha yake ya kawaida. Aliwakumbuka sana watoto wake Mahangaiko na Shida. Huko walikokwenda, Mahangaiko na Shida walitumia pesa zote zikaisha hatimaye wakaishi maisha ya shida mno. Walijutia matendo yao wakarudi nyumbani na kumtaka radhi mama yao.

**Maswali**

41. Andika kichwa kinachofaa kwa hadithi uliyoisoma?
42. Mwandishi anamaanisha nini akisema "alikata kamba?"
43. Kwa nini Chakupewa alichuma majani na kudondosha njiani wakati wa kwenda msituni?
44. Nini kilisababisha kifo cha Mzee Beberu?
45. Hadithi hii inatufundisha nini katika maisha yetu ya kila siku?





Scanned with CamScanner